TUME YA HUDUMA ZA JAMII YA KIKRISTO (CSSC)

KAMATI YA MTIHANI WA PAMOJA KANDA YA KASKAZINI

MTIHANI WA UTAMIRIFU - KIDATO CHA PILI, AGOSTI 2026

060 HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

MWONGOZO WA USAHISHAJI (CSSC)

1.

i	ii	iii	iv	v	vi	vii	viii	ix	x
C	B	A	C	D	C	A	B	D	A

Alama01 @= Alama10

2.

i	ii	iii	iv	v
C	F	A	D	B

Alama01 @= Alama05

3. MTAHINIWA ANATAKIWA KUFAFANUA SABABU ZILIZOPELEKEA MAPINDUZI MATUKUFU YA ZANZIBARI.

i. **Utawala wa wachache** Madaraka yalikuwa mikononi mwa kundi dogo la Waarabu na Wasultani, huku Waafrika walio wengi wakinyimwa ushawishi wa kisiasa.

ii. **Udhalimu na ubaguzi** Kulikuwa na ubaguzi wa rangi na kijamii, ambapo Waafrika walipata haki na fursa chache kuliko makundi mengine.

iii. **Ukosefu wa haki katika uchaguzi** Uchaguzi wa mwaka 1963 ulidaiwa kutokuwa wa haki, kwani chama kilichopata kura nyingi hakikupewa nafasi ya kuunda serikali.

iv. **Kutokuwepo kwa njia za amani za kuleta mabadiliko** Malalamiko ya wananchi hayakushughulikiwa ipasavyo, hivyo wengi wakaamini mapinduzi ndiyo njia pekee ya kuondoa utawala uliokuwepo.

v. **Kunyang'anywa haki za kiuchumi** Ardhi, biashara na utajiri mkubwa vilimilikiwa na watu wachache, hali iliyozua chuki na kutoridhika miongoni mwa wananchi wengi.

vi. **Hamasa na uongozi wa vyama vya ukombozi** Viongozi na wanachama wa vyama vya kisiasa, hasa ASP, walihamasisha wananchi kupigania mabadiliko ya kweli.

vii. **Shinikizo la kupata uhuru kamili** Baada ya uhuru wa mwaka 1963, wananchi wengi waliona bado kulikuwa na mfumo wa utawala usiowawakilisha walio wengi, hivyo walitaka kuondoa kabisa utawala huo kupitia Mapinduzi ya mwaka 1964.

Alama 02 @ = 10

4. MTAHINIWA ANATAKIWA KUTAJA MADHARA YA RUSHWA

i. **Huvunja haki na usawa** Wenye uwezo wa kutoa rushwa hupata huduma haraka kuliko wasioweza.

ii. **Hupunguza uaminifu kwa serikali na taasisi za umma** Wananchi hupoteza imani kuwa watatendewa haki.

iii. **Huchelewesha huduma kwa wasiotoa rushwa** Watu wasio na fedha hulazimika kusubiri kwa muda mrefu.

iv. **Huongeza vitendo vya ufisadi** Watumishi wengine huiga tabia hiyo na kuifanya kuwa kawaida.

v. **Hudhoofisha maendeleo ya nchi** Rasilimali na huduma hazitolewi kwa haki, hivyo maendeleo huathirika.

vi. **Husababisha umaskini na gharama zisizo za lazima** Wananchi hulazimika kutumia fedha zaidi ili kupata huduma wanazostahili.

vii. **Huvunja maadili na sheria Rushwa** ni kinyume cha sheria na hujenga utamaduni wa kutokuwa waaminifu katika jamii.

Alama 02 @ = 10

5. MTAHINIWA ANATAKIWA KUELEZA SABABU ZA MATAIFA YA ULAYA KUJA BARANI AFRIKA

i. **Kutafuta malighafi** Nchi za Ulaya zilihitaji malighafi kama pamba, mpira, dhahabu, shaba na mafuta kwa ajili ya viwanda vyao.

ii. **Kutafuta masoko ya bidhaa** Zilitafuta sehemu za kuuza bidhaa zilizotengenezwa viwandani kwa kuwa masoko ya Ulaya yalikuwa hayatoshi.

iii. **Kutafuta maeneo ya uwekezaji** Wawekezaji wa Ulaya walihitaji maeneo ya kuwekeza mitaji yao na kupata faida.

iv. **Kutafuta nguvu kazi** Walihitaji wafanyakazi wa bei nafuu wa kufanya kazi katika migodi, mashamba na miradi mingine ya kiuchumi.

v. **Kueneza dini ya Kikristo** Wamisionari walikuja kuhubiri Ukristo na kuanzisha shule pamoja na hospitali.

vi. **Mashindano ya kikoloni na kuongeza himaya Mataifa** ya Ulaya yalishindana kutawala maeneo mengi zaidi ili kuongeza nguvu na hadhi zao duniani.

vii. **Kuchunguza na kugundua maeneo mapya** Wapelelezi na wagunduzi walifika Afrika kutafuta taarifa za kijiografia, njia za biashara, mito, madini na fursa nyingine za kiuchumi.

Alama 02 @ = 10

6. MTAHINIWA ANATAKIWA KUELEZA SABABU ZA JAMII ZA ASILI YA TANZANIA KUPINGA UJIO WA WAKOLONI

i. **Kupoteza Uhuru wa Kisiasa na Mamlaka**
Kabla ya ukoloni, kila jamii ilikuwa na mfumo wake wa uongozi chini ya Machifu, Mitemi, au Masultani. Wakoloni walipofika, waliwapokonya viongozi hawa madaraka na kuanzisha mifumo mipya.

ii. **Unyang'anyaji wa Ardhi**
Ardhi ilikuwa mali ya jamii na msingi wa maisha (kilimo na ufugaji). Wakoloni walichukua maeneo yenye rutuba na kuwapa walowezi wa kizungu au kuanzisha mashamba makubwa ya mkonge na pamba.

iii. **Kazi za Shuruti (Manamba)**
Ili kuendesha uchumi wao, wakoloni waliwalazimisha Waafrika kufanya kazi ngumu kwenye mashamba ya mkonge, ujenzi wa reli, na barabara.

iv. **Kodi Kandamizi (Kodi ya Kichwa na Nyumba)**
Wakoloni walianzisha kodi za lazima ili kuwalazimisha Waafrika waingie kwenye mfumo wa fedha na kufanya kazi kwa wazungu. Wale walioshindwa kulipa kodi walipigwa, walidhalilishwa mbele ya familia zao, au nyumba zao zilichomwa moto

v. **Dharau Dhidi ya Utamaduni na Dini za Asili**
Wamisionari na maofisa wa kikoloni walidharau mila, desturi, na imani za kijadi za Waafrika, wakiziita kuwa ni za "kishenzi." Kwa mfano, walipiga marufuku baadhi ya matambiko na kuharibu maeneo matakatifu.

vi. **Unyanyasaji na Ukatili wa Maofisa wa Kikoloni**
Maofisa wa ngazi za chini (kama Maakida na Majumbe nchini Tanganyika) walikuwa na tabia ya kutesa wananchi, kuchukua mifugo yao, na hata kuwadhalilisha wanawake.

vii. **Kulinda Biashara na Uchumi wa Ndani**
Baadhi ya jamii, kama Wayao na Wanyamwezi, walikuwa wamefika mbali katika biashara ya masafa marefu. Ujio wa wakoloni uliingilia njia hizi za biashara na kuweka ukiritimba uliowazuia Waafrika kufaidika na rasilimali zao.

Alama 02 @ = 10

7. **MTAHINIWA ANATAKIWA KUFAFANUA JINSI SANAA NA MICHEZO ILIVYOTUMIKA KAMA NJIA MBADALA YA KUDAI UHURU.**

i. **Kuamsha uzalendo** Nyimbo, ngoma na maigizo yaliwahamasisha wananchi kuipenda nchi yao na kutaka kujitawala.

ii. **Kuelimisha wananchi** Sanaa ilitumika kutoa elimu kuhusu madhara ya ukoloni na umuhimu wa kupigania uhuru.

iii. **Kuunganisha wananchi** Michezo na shughuli za sanaa ziliwaleta pamoja watu wa makabila na dini tofauti katika lengo la kudai uhuru.

iv. **Kueneza ujumbe wa uhuru Nyimbo**, mashairi na maigizo vilisambaza ujumbe wa kupinga ukoloni na kuhimiza mshikamano.

v. **Kujenga ujasiri na moyo wa kupambana** Sanaa na michezo viliongeza ari, matumaini na ujasiri wa wananchi katika harakati za kudai uhuru.

vi. **Kukusanya watu kwa mikutano** Mashindano ya michezo na maonesho ya sanaa yalitumika kama fursa ya kukusanya wananchi na kuwafikishia ujumbe wa kisiasa kwa urahisi.

vii. **Kuimarisha umoja wa kitaifa** Sanaa na michezo zilisaidia kuondoa tofauti za kikabila na kuimarisha mshikamano wa Watanganyika katika kudai uhuru.

Alama 02 @ = 10

8. **MTAHINIWA ANATAKIWA KUTAJA SABABU ZILIZOPELEKEA KUKUA KWA UCHUMI KWENYE JAMII ZA ASILI YA TANZANIA.**

i. **Kilimo** Kiliongeza uzalishaji wa chakula na mazao ya biashara kwa kubadilishana.

ii. **Ufugaji** Ulichangia upatikanaji wa chakula, ngozi, maziwa na mali kwa ajili ya biashara.

iii. **Biashara** Biashara ya ndani na ya masafa marefu ilichochea ubadilishanaji wa bidhaa na kuongeza utajiri.

iv. **Uvuvi** Ulitoa chakula na bidhaa za kuuzwa au kubadilishana na jamii nyingine.

v. **Uwindaji na ukusanyaji** Vilitoa chakula, ngozi, pembe na bidhaa nyingine za matumizi na biashara.

vi. **Maendeleo ya teknolojia ya zana Utengenezaji** wa zana za chuma na vifaa vingine uliimarisha kilimo, uwindaji na shughuli nyingine za uzalishaji.

vii. **Amani na ushirikiano kati ya jamii Hali** ya amani iliwezesha watu kufanya shughuli za kiuchumi na biashara bila vikwazo vikubwa.

Alama 02 @ = 10

9. MTAHINIWA ANATAKIWA KUTAJA ATHARI ZA VITA ZA MAJIMAJI

i. **Vifo vya Watu Wengi:** Inakadiriwa kuwa zaidi ya Waafrika 250,000 hadi 300,000 walipoteza maisha. Wengi wao hawakufa kwa risasi tu, bali pia kwa njaa iliyosababishwa na mbinu ya Wajerumani ya kuchoma moto mashamba na mazingira

ii. **Janga la Njaa na Umaskini:** Wajerumani waliteketeza akiba ya chakula, kuchoma moto nyumba, na kuharibu mashamba ili kuwanyima wapiganaji chakula. Hali hii ilisababisha njaa kubwa iliyodumu kwa miaka kadhaa baada ya vita.

iii. **Kuvunjika kwa Mfumo wa Kijamii na Kiuchumi:** Jamii nyingi za Kusini mwa Tanzania zilitawanywa, familia zilitenganishwa, na shughuli za kawaida za kiuchumi kama kilimo na biashara ziliahirishwa au kuharibiwa kabisa.

iv. **Uharibifu wa Mali:** Miji, vijiji, vituo vya Wajerumani, na miundombinu ya usafirishaji viliharibiwa vibaya wakati wa mapigano.

v. **Kupoteza Uongozi wa Asili:** Viongozi wengi wa kimila na waliowezesha uasi huo (kama vile Kinjeketile Ngwale na viongozi wengine wa kabila) walikamatwa na kunyongwa na serikali ya Kijerumani, jambo lililoacha ombwe kubwa la uongozi.

Alama 02 @ = 10

10. MTAHINIWA ANAKIWA KUFAFANUA VICHOCHEO VYA MABADILIKO YA SAYANSI NA TEKINOLOJIA KABLA YA UKOLONI.

Utangulizi Alama 02½

Sayansi: ni mchakato wa kupata maarifa kuhusu mazingira na dunia kwa kutumia uchunguzi, majaribio, utafiti na uthibitisho wa ukweli.

Teknolojia: ni matumizi ya maarifa ya kisayansi na ujuzi wa binadamu kubuni, kutengeneza au kuboresha zana, vifaa na mbinu za kutatua matatizo na kurahisisha maisha ya watu.

Kiini cha swali Alama @ 02

i. **Mahitaji ya kijamii** Changamoto za makazi, mavazi, usafiri na upatikanaji wa chakula zilihamasisha ubunifu na uvumbuzi wa teknolojia mpya.

ii. **Biashara na ushirikiano** Ilihamasisha utengenezaji wa bidhaa bora na kuboresha njia za usafiri na mawasiliano.

iii. **Rasilimali za asili** jamii nyimgi zilikuwa na utajiri wa rasilimali za asili kama vile madini, mbao mazao na wanyamapori iliyopelekea uvumbuzi wa mbinu za utunzaji bora wa rasilimali hizo.

iv. **Utaratibu wa kijamii** ulichochea uvumbuzi wa tekinolojia ushirikiano kati ya wanajamii na wataalamu wa kijadi ulikuwa muhimu katika kujenga na kuboresha tekinolojia.

v. **Uvumbuzi wa kijadi** jamii zilikuwa na uvumbuzi wa kiasili unaotokana na ujuzi wa kijadi na maarifa ya asili, hii ilijumuisha mbinu za kilimo, utengenezaji wa vyombo vya nyumbani nk.

vi. **Elimu ya jadi** jamii za kitanzania zilikuwa na utajiri wa maarifa ya asili yaliyohusiana na mazingira historian a utamaduni, maarifa haya yalikua msingi wa ufahamu wao wa ulimwengu.

vii. **Ongezeko la idadi ya watu** Lilisababisha hitaji la kuboresha uzalishaji wa chakula na zana za kazi.

viii. **Ugunduzi wa chuma** Uliwezesha utengenezaji wa zana na silaha zenye ubora zaidi

Hitimisho Alama 02½

Kwa ujumla, mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika jamii za asili kabla ya ukoloni yalitokana na mahitaji ya maisha ya kila siku, kama vile kilimo, biashara, ulinzi, ongezeko la watu na mwingiliano kati ya jamii. Mabadiliko hayo yaliwezesha kuboreshwa kwa uzalishaji, kurahisisha maisha ya watu na kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika jamii za asili za Tanzania.